

Jina.....

Nambari.....

Shule.....

Sahihi.....

Tarehe.....

102/3

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**(FASIHI)**

**JULAI/ AGOSTI**

**Muda : saa 2 ½**

**MTIHANI YA PAMOJA WA WILAYA YA MANGA -2012**  
**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SHULE YA UPILI**

102/3

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**(FASIHI)**

**JULAI/ AGOSTI**

**Muda : saa 2 ½**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

- (a) Jibu maswali manne pekee
- (b) Swali la kwanza ni la lazima
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani :  
Riwaya, Tamthlia, Ushairi na Hadithi fupi.
- (d) Usijibu maswali mawali kutoka sehemu moja.
- (e) Kila swali lina alama 20.
- (f) Mtihani huu una alama 80.

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa*

*Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

### **SEHEMU A:FASIHI SIMULIZI**

1. (a) Nini maana ya Miviga? (al.2)
- (b) Fafanua sifa zozote tano za miviga kashi ueleze dhima yake katika jamii (al.10)
- (c) Elezea sifa zinazotambulisha muundo wa nyimbo (al.8)

### **SEHEMU B.Utengano S.a Mohamed.**

2. Huko ukitolea mifano kutoka kitabuni, elezea migogoro mbalimbali inayojitokeza katika riwaya ya utengano. (al.20)
3. Mabadiliko sasa, alisema kwa kinywa kipana, kasha-----
  - (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (al.4)
  - (b) Taja na uelezee tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (al.3)
  - (c) Mbali na mhusika anayerejelewa katika dondoo hili, taja wahusika wowote wawili kisha uelezee mabadiliko yaliyowapata.

### **SEHEMU C: Kifo Kisimani .K Mberia**

4. (a) Thibisha kauli kuwa mwandishi wa tamthilia ya kifo kisimani amefaulu katika kutumia mbinu ya jazanda.
- (b) Kwa kutolea mifano mwafaka onyesha ufaafu wa anwani 'Kifo Kisimani' ukirejerea tamthilia husika (al.14)

### **SEHEMU D.Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine K.W Wamitila**

5. Mwanamke amesawiriwaje katika hadithi zifuatazo
  - (a) Uteuzi wa moyoni
  - (b) Ngome ya nafsi
6. Hadithi ya Mkimbizi ni kioo cha matukio yanayotokea katika nchi za kiafrica.Fafanua athari za vita vya kikabila kwa mujibu wa hadithi hii.
7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata  
Mkata ni mkatika,haridhi hatoridhiwa  
Sina ninaloshika,wala ninalochukuwa  
Mlimwengu kanipoka,hata tone la muruwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina ng'ombe wa mbuzi ,sina konde sina buwa  
Sina hata makazi,mupasayo kuyajua  
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa  
Mirithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa  
Sina chembe ya majazi,mno nikukamuliwa  
Nikwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa  
Mrithi nini mwanangu?

Sina sikuachi jina,mkata hatasifiwa  
Hata nifanye la mana,mno ni kulaumiwa  
Poleni wangu sana, sina kwenu cha kutowa  
Mrithi nini mwanangu?

Sina leo sina jana ,sina kesho kutwaaliwa  
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa  
Sina wanangu mi sina,sina la kuacha kuraduwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki,mila yangu meuliwa  
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa  
N'nawaua na miliki,hadi nitakapofukiwa  
Mirithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu,wenye kulongowa  
Muwane kwa nyingi mbinu,Mwende pasi kupumuwa  
Leo siye kesho yenu,kama mutajikamuwa  
Mrithi nini wanangu?

- (a) Kwa kuzingatia kibwagizo ,hili ni shairi gani? (al.2)
- (b) Eleza sababu ya mtunz kutoweza kuwarithisha wanawe (al.3)
- (c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari (al.4)
- (d) Dondoa mifano miwilimiwili ya

- (i) Inkisari
- (ii) Tabdila (al.4)
- (e) Chambua shairi hili kiarudhi (al.5)
- (f) Eleza maana ya vifungu hivi (al.2)
  - (i) Mlimwengu kanipoka
  - (ii) Sina konde sina buwa